# WILAYA YA BUSIA

# DARASA LA NNE MUHULA WA TATU

# KISWAHILI

PENPLUS BUSIA

***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***Jaza mianya kwa jibu sahihi.***

Siku __1__ Linda na wazazi __2__ walienda Ngomeni kutembelea sehemu za makao __3__ wanyama wa pori. Ilikuwa siku ya Jumamosi, Linda __4__ wazazi __5__ walipoanza safari. Jumapili wakafika mahali __6__. Kulikuwa na wanyama __7__ aina __8__. Mifano ya wanyama __9__ ni nguruwe mwitu, swala, nyati na tumbili.

Tumbili ni __10__ mtundu sana. __11__ hupenda kuchezea watu. Linda alikuwa na __12__ ya soda mkononi. Tumbili naye alikuwa kando __13__ ya mti. Akashuka pole pole akampokonya __14__ mtoto chupa ya soda __15__ kutoroka.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mmoja | B. moja | C. kimoja | D. kimoje |
| 2. | A. wake | B. chake | C. yake | D. mwake |
| 3. | A. lake | B. nake | C. huu | D. ya |
| 4. | A. cha | B. na | C. na | D. lao |
| 5. | A. wao | B. wa | C. wako | D. wake |
| 6. | A. huko | B. hao | C. huo | D. hicho |
| 7. | A. ya | B. wa | C. cha | D. za |
| 8. | A. nyingi | B. wa | C. kingi | D. nyingine |
| 9. | A. hao | B. mwingi | C. huyo | D. chao |
| 10. | A. kinyama | B. mnyama | C. wanyama | D. unyama |
| 11. | A. Wewe | B. Mnyama | C. Wao | D. Yeye |
| 12. | A. vyumba | B. wingi | C. nyupa | D. chupa |
| 13. | A. chatu | B. vyupa | C. juu | D. ndani |
| 14. | A. yule | B. dani | C. kile | D. vile |
| 15. | A. nao | B. na | C. wa | D. kwa |

***Kutoka swali la 16-30, chagua jibu kulingana na maagizo ulivopewa***


16. Chagua majina yaliyo katika ngeli ya U-I
   A. Mbwa, mtoto, mswaki
   B. Mtu, mchezo, mpira
   C. Mchezo, mpira, mswaki
   D. Mtoto, mtu, mchezo

17. ***Wingi wa sentensi hii ni***
   Mgeni aliwasili nyumbani
   A. Mgeni waliwasili nyumbani.
   B. Wageni waliwasili nyumbani
   C. Wageni waliwasili manyumbani.
   D. Wageni aliwasili nyumbani

18. ***Kamilisha sentensi kwa silabi inayofaa.***
   Magurudumu ________ mebadilishwa
   A. ya    B. li
   C. ma    D. i

19. Bendera ya Kenya ina rangi zipi?
   A. Nyeusi, nyekundu, kijani, kinjano
   B. Nyeusi, nyekundu, nyeupe, kijani
   C. Nyekundu, nyeusi, kijani, kinjano
   D. Nyeupe, nyeusi, nyekundu, kahawia

20. Andika jina la umbo hili.



   A. mraba
   B. pia
   C. mviringo
   D. mstatili

21. Taja vifaa vinavyotumika shambani.
   A. Uteo, mwiko, jembe, rato
   B. Rato, jembe, mkuki, sinia
   C. Mbuzi, seredani, beleshi, jembe
   D. Jembe, reki, panga, rato

22. ***Kamilisha methali hii:***
   Mti upigwao mawe ni wenye ________
   A. ndege    B. matawi    C. matunda    D. kuni

23. Andika nambari hii kwa maneno 915.
   A. Mia tisa na kumi na tano
   B. Mia sita na kumi na tano
   C. Mia tisa na tano
   D. Mia tano kumi na tisa

24. Jibu la maamkizi haya ni yapi? Shikamoo ________
   A. hujambo    B. salama
   C. marahaba    D. habari

25. ***Jaza kwa neno lifaalo.***
   Nyanya hukaa kwenye ________ anapotusimulia hadithi.
   A. jiko    B. kigoda    C. bafu    D. choo

26. ***Kanusha sentensi hii:***
   Mama amepika chakula kitamu.
   A. Mama hatapika chakula kitamu
   B. Baba hajapika chakula kitamu
   C. Mama wamepika chakula kitamu
   D. Mama hajapika chakula kitamu

27. ***Tumia kiulizi ngapi vizuri katika sentensi.***
   Mikate ________ ngapi imepakwa siagi?
   A. tu    B. mi    C. ma    D. m

28. ***Tegua kitendawili hiki.***
   Mama yangu daima hachoki kunibeba ________
   A. kitanda    B. mama
   C. mtoto    D. mkoba

29. Andika vinyume vya maneno yaliyoko hapa chini

| | **baridi** | **ghali** | **faida** | **taratibu** |
|---|---|---|---|---|
| A. | Joto | ngumu | hasara | polepole |
| B. | Joto | rahisi | pesa | haraka |
| C. | Joto | rahisi | hasara | haraka |
| D. | Joto | ngumu | pesa | haraka |

30. Panga vile maneno haya yatakuwa katika kamusi.
magadi, mafua, madhara
A. Madhara, mafua, magadi
B. Mafua, madhara, magadi
C. Mafua, magadi, madhara
D. Magadi, mafua, madhara

***Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali yanayofuata 31-40.***

Nyani alikuwa akiishi juu ya mwembe karibu na mto. Alikuwa na rafiki yake aliyeitwa Mamba. Mamba aliishi mtoni. Wao walikuwa marafiki wa chanda na pete. Kila siku, nyani alikuwa akimpa mamba zawadi ya maembe.

Mamba aliyachukua maembe na kuyapelekea mke wake huko mtoni. Lakini mke wa mamba alikuwa na roho mbaya.

Siku moja, mke wa mamba alijifanya ni mgonjwa sana. Mume wake akamletea kila aina ya dawa lakini hakupona. Mke wa mamba akamwambia mumewe "ikiwa wewe unanipenda kweli basi dawa yangu ni kula moyo wa nyani. Nikila moyo wa nyani nitapona. Nenda kamwalike rafiki yako nyani, akifika hapa tutamuua, nami nitakula moyo wake."

Mamba hakujua la kufanya. Alishindwa kuamua kati ya kumpendeza mke wake au kuendeleza urafiki wake na nyani. Alitatizika.

31. Nyani na mamba walikuwa wakiishi wapi?
A. Juu ya mwembe B. Juu ya mwembe na mtoni
C. Mtoni D. Mtoni na juu ya mwembe

32. Rafiki yake nyani alikuwa nani?
A. Mke wa nyani B. Mke wa mamba
C. Nyani D. Mamba

33. Marafiki wa chanda na pete ni marafiki wa aina gani?
A. Marafiki wabaya B. Marafiki wazuri
C. Marafiki wawili D. Marafiki wakubwa

34. Mke wa mamba alikuwa na sifa gani?
A. Kuua B. Kupenda C. Kucheza D. Kupika

35. Ni nini umoja wa neno maembe?
A. Mwembe B. Embe
C. Tunda D. Matunda

36. Je, unafikiri mke wa mamba alikuwa mgonjwa?
A. Ndio B. Hapana C. La D. Hatujaambiwa

37. Ni nani alitaka kula nyama ya moyo?
A. Mamba B. Nyani
C. Mke wa mamba D. Mke wa nyani

38. Mamba aliyafanyia nini maembe aliyopewa?
A. Kuyala B. Kuyatupa
C. kuyauza D. kumpa mkewe

39. Ni nini maana ya "alitatizika?"
A. Alichanganyikiwa B. Alikataa
C. Alikatazwa D. Alipotea

40. Hadithi hii inatufunza ______
A. tuwe marafiki wabaya B. tuwe marafiki wa kweli
C. tuuane D. tusiwe na marafiki

***Soma hadithi hii kisha ujibu swali la 41-50.***

Safari ya garimoshi iliharibika. Garimoshi liliacha njia ya reli na kupinduka. Watu wachache walikufa. Siku yenyewe ilikuwa ni ya baridi kali.

Baada ya muda, mabasi yakaja. Mabasi hayo yaliletwa kuwasaidia wasafiri wa garimoshi. Wasafiri hao wakaanza kupakia mizigo yao katika mabasi. Mabasi yatawapeleka huko walikokuwa wanaenda.

Kulikuwa na bibi mmoja katika ajali hiyo. Ajuza huyo alikuwa na mjukuu wake na mzigo mzito. Wasafiri walishindana kupanda mabasi. Kila mmoja alikuwa akipigania nafasi ya kuingia.

Ajuza huyo hakujua afanye nini kati ya kubeba mzigo au kumchunga mjukuu wake. Hakuweza kufanya yote hayo kwa pamoja. Aliogopa kumpoteza mjukuu au kuupoteza mzigo wake.

Kulikuwa na manamba wawili katika basi moja. Mmoja wa manamba hao alikuwa kijana. Aliwasaidia wasafiri wengi kwa kuwabebea mizigo yao na kuwapandishia kwenye basi. Barobaro huyo alikuwa anaitwa Masha. Masha alimuona ajuza akiwa na wasiwasi. Papo hapo akambebea mzigo wake yule ajuza na kumwekea kwenye basi. Ajuza alitiririkwa na machozi.

41. Kwa nini safari iliharibika?
A. Gari halikuja B. Garimoshi lilipinduka
C. Dereva hakuja D. Wasafiri hawakuja

42. Watu wangapi walikufa?
A. Wawili B. Wengi C. Wachache D. Mmoja

43. Ajuza ni nani?
A. Babu B. Msafiri C. Dereva D. Nyanya

44. Ni nini ilikuja kuwasaidia wasafiri?
A. Mabasi B. Madereva C. Manamba D. Magari

45. Ajuza alikuwa na ______ na ______
A. machozi, mizigo B. kijana, mizigo
C. mizigo, mtoto D. mzigo, mjukuu

46. Ajuza hakutaka kupoteza ______ na ______
A. gari, basi B. mjukuu, mzigo
C. njia, mzigo D. pesa, mzigo

47. Kwa nini ajuza alitiririkwa na machozi?
A. Huzuni B. Furaha
C. Kuchoka D. Kupoteza mzigo

48. Ni nani alimsaidia ajuza kubeba mzigo?
A. Masha B. Msafiri C. Dereva D. Mjukuu

49. Garimoshi hupitia kwenye ______
A. barabara B. angani C. reli D. majini

50. Ni nani walishindana kuingia na kupanda mabasi?
A. Madereva B. Manamba C. Wasafiri D. Kijana